



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA
BARAZA LA FAMASI**



TAARIFA KWA UMMA

UFAFANUZI WA HOJA ZA BARUA YA WAZI KWA MH. WAZIRI WA AFYA KUHUSU USAJILI WA WANAFUNZI AMBAO BADO WAKO CHUONI NA WASIO NA VIGEZO

DODOMA: 10 Aprili, 2026

Mnamo tarehe 09 Aprili, 2026, Wizara ya Afya ilipokea kwa njia ya mitandao ya kijamii barua ya wazi iliyoelekezwa kwa Mhe. Waziri wa Afya kuhusu wanafunzi wa ufamasia na udaktari wanaosoma nje ya nchi ambao bado hawajahitimu na wasiokuwa na vigezo kusajiliwa kutoa huduma za afya nchini. Tuhuma zilizoibuliwa kwenye barua hiyo ni kama ifuatavyo;

- i. Uwepo wa wanafunzi ambao hawakufaulu Kidato cha Nne na Sita lakini wana Shahada za Udaktari na Ufamasia na wameidhinishwa na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Baraza la Famasi Tanzania (PCT) na Baraza la Madaktari Tanganyika (MCT);
- ii. Wanafunzi waliofeli Kidato cha Sita kutoa fedha TCU na kupelekwa India kusoma ufamasia na wote kusajiliwa na Baraza la Famasi na sasa wako kwenye kazi wanahudumia wananchi;
- iii. Uwepo wa kundi la vijana waliopo nchini India wanaoendelea na masomo ya ufamasia na wanachanga pesa ili kuhonga TCU pamoja na mabaraza wasajiliwe kabla ya kumaliza masomo; na
- iv. Wanafunzi ambao hawajafaulu wanapofika nchini India na China hulipa fedha na kupewa shahada kabla ya kumaliza muda wa masomo husika.

Kufuatia tuhuma hizo, Baraza la Famasi linatoa ufafanuzi kama ifuatavyo:

Baraza la Famasi linatekeleza majukumu yake kwa kufuata taratibu zilizoainishwa kwenye Sheria na Kanuni zinazosimamia taaluma ya famasi ili kuhakikisha wanataaluma wenye vigezo na umahiri unaohitajika ndio wanaosajiliwa kutoa huduma kwa lengo la kulinda afya za wananchi.

Katika kusajili wahitimu, Baraza linazingatia sifa na vigezo kama zilivyoainishwa katika kifungu cha 14 (1)(2) na 16 (1)(2) cha Sheria ya Famasi, Sura 311 Marejeo ya 2023 na kanuni ya 5 na 10 ya Kanuni za Usajili, Uandikishaji na Uorodheshaji wa Wanataaluma za Mwaka 2005 na Kanuni ya 4 (1) ya Kanuni za Elimu na Mafunzo za Mwaka 2005.

pharmacy_council_tanzania Pharm_council www.pc.go.tz Pharmacy Council-Tanzania



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA AFYA
BARAZA LA FAMASI**



Baraza la Famasi limekuwa likitekeleza majukumu yake bila ushawishi wa aina yoyote. Hata hivyo, Baraza linaendelea kufuatilia kwa karibu hoja zilizoibuliwa ili kuhakikisha wahitimu wanaosajiliwa ni wale wenye sifa stahiki.

Baraza linawahakikishia wananchi kuwa litaendelea kusimamia taaluma ya famasi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo ili kulinda afya ya jamii. Aidha, Baraza linatoa wito kwa wanafunzi wanaotaka kujiunga na mafunzo ya shahada ya famasi kufuata miongozo inayotolewa na mamlaka za usimamizi na udhibiti wa elimu na taaluma nchini.

Imetolewa na:

**Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma
BARAZA LA FAMASI**

pharmacy_council_tanzania Pharm_council www.pc.go.tz Pharmacy Council-Tanzania